# HALMASHAURI YA WILAYA MPANDA

Tel: Fax 025-2820068
Fax No. 025-2820068
Email – dedtanganyika@go.tz

S.L.P 1,
**MPANDA.**
22/11/2021

Mahali: PMU MAJALILA

**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KUPITIA NA KUTUNUKU ZABUNI ZA MAFUNDI KWA AJILI YA UJENZI WA WODI TATU AMBAZO NI WODI YA WANAUME, WODI YA WANAWAKE NA WODI YA WATOTO CHA TAREHE 22/11/2021 KATIKA UKUMBI WA HOSPITALI MAJALILA.**

**WALIOHUDHURIA:**

| Na. | JINA | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | HALIMA KITUMBA | M/KITI |
| 2 | HARSON H. TEMU | KATIBU |
| 3 | DOTTO S.KWIGEMA | MJUMBE |
| 4 | MICHAEL LYAMBILO | MJUMBE |
| 5 | HIMIDI OMARI | MJUMBE |
| 6 | BETUELY RUHEGA | MJUMBE |
| 7 | KAGEMLO MUTAGWABA | MWANASHERIA |
| 8 | ALPHONCE KALOBELO | SEKRETARIETI |
| 9 | SALUM IBRAHIM | MWALIKWA |
| 10 | MUSA KACHELE | IDARA TUMIZI |

**AGENDA**

1) Kufungua kikao
2) Kudhibitisha agenda
3) Uteuzi wa wajumbe wapya wa Bodi ya Zabuni
4) Kusoma na kupitisha Muhtasari wa kikao kilichopita
5) Kupitia na kutunuku zabuni za mafundi za ujenzi wa wodi tatu
6) Miradi ya UVICO-19
7) Mengineyo kwa idhini ya M/Kiti
8) Kufunga kikao

**AGENDA NA. HW/KTV/01/22/11/2021 – KUFUNGUA KIKAO:**

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 3:30 asubuhi. M/Kiti alielekeza mtaalamu wa ujenzi awepo kwa msaada wa kitaalamu Zaidi pamoja na idara tumizi ili kupata taarifa sahihi juu ya utekelezaji wa ujenzi husika.



Scanned with CamScanner

**AGENDA NA. HW/KTV/02/22/11/2021 – KUDHIBITISHA AGENDA:**
Agenda zilisomwa na katibu na wajumbe waliridhia agenda hizo zitumike kama zilivyo kwa ajili ya kikao.

**AGENDA Na. HW/KTV/04/22/11/2021 – KUSOMA NA KUPITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA.**
Muhtasari wa kikao kilichopita ulipitiwa na wajumbe kwa pamoja kurasa kwa kurasa na marekebisho machache ya kimaandishi yalipitiwa na kuridhiwa kuwa muhtasari usainiwe kwa ajili ya kuwa kumbukumbu za Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika.

**AGENDA NA. HW/KTV/03/22/11/2021 – UTEUZI WA WAJUMBE WA BODI YA ZABUNI:**
Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe wapya walioteuliwa na Mkurugenzi wa Halmashauri na kuthibitishwa na kikao cha kamati ya fedha uongozi na mipango kilichoketi 15/11/2021 kuwa wajumbe halali wa bodi ya zabuni kwa kipindi cha miaka mitatu. Wafuatao ndio wajumbe walioteuliwa na kuithinishwa

| Na. | JINA | WADHIFA | CHEO |
|---|---|---|---|
| 1 | HARSON H. TEMU | KATIBU | Afisa Manunuzi na Ugavi |
| 2 | DOTTO S.KWIGEMA | MJUMBE | Afisa Mipango |
| 3 | MICHAEL LYAMBILO | MJUMBE | Afisa Elimu Sekondari |
| 4 | BETUELY RUHEGA | MJUMBE | Afisa Utumishi |
| 5 | KAGEMLO MUTAGWABA | MWANASHERIA | Mwanasheria |

**AGENDA NA. HW/KTV/05/22/11/2021 – KUPITIA NA KUTUNUKU KAZI ZA MAFUNDI KWA AJILI YA UJENZI WA WODI TATU.**

Katibu aliwasilisha mapitio ya taarifa ya timu ya upembuzi “evaluation report” kwa kuzingatia mpangilio wa zabuni ulivyotangazwa na gharama zilizoainishwa kwa mafundi husika. Aidha mapendekezo ya timu ya upembuzi yanapendekeza kuwa mafundi wote wapatiwe kazi na baada ya kitengo cha manunuzi kupitia kimeafiki mapendekezo hayo kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo;



Scanned with CamScanner

| Na. | JINA LA ZABUNI | NAMBA YA ZABUNI |
|---|---|---|
| 01 | UMALIZIAJI WA UJENZI WA JENGO LA WANAWAKE | TDC/DH/W/FA/2021/2022/06 |
| 02 | UMALIZIAJI WA UJENZI WA JENGO LA WANAUME | TDC/DH/W/FA/2021/2022/07 |
| 03 | UJENZI WA JENGO LA WODI YA WANAUME | TDC/DH/BLG/FA/2021/2022/02 |
| 04 | UJENZI WA JENGO LA UPASUAJI | TDC/DH/BLG/FA/2021/2022/03 |
| 05 | UJENZI WA JENGO LA KUHIFADHIA MAITI | TDC/DH/BLG/FA/2021/2022/04 |
| 06 | UMALIZIAJI WA UJENZI WA JENGO LA WATOTO | TDC/DH/W/FA/2021/2022/08 |

**AZIMIO**

Kikao kiliazimia yafuatayo;

Mafundi waliiomba kazi za umaliziaji wa wodi tatu wasipewe kazi hizo kutokana na kushindwa kukamilisha kazi zao pindi walipopatiwa mkataba ambao umesitishwa. Mafundi hao ni hawa wafuatao;

| Na. | JINA LA ZABUNI | NAMBA YA ZABUNI | JINA LA MZABUNI |
|---|---|---|---|
| 01 | UMALIZIAJI WA UJENZI WA JENGO LA WANAWAKE | TDC/DH/W/FA/2021/2022/06 | JACKSON CHAMBALA |
| 02 | UMALIZIAJI WA UJENZI WA JENGO LA WANAUME | TDC/DH/W/FA/2021/2022/07 | NASHON M. PETER |
| 03 | UMALIZIAJI WA UJENZI WA JENGO LA WATOTO | TDC/DH/W/FA/2021/2022/08 | TITUS J. LUGOYE |

Kikao kimeelekeza kuwa mchakato wa kumpata fundi mwingine uanze mara moja kwa kutumia njia ya single source ama competitive quotations ili kuharakisha upatikanaji wa fundi kwani ni muda mrefu sasa miradi ile imesimama.

**AGENDA NA. HW/KTV/06/22/11/2021 – MIRADI YA UVICO 19**

Kikao kilijadili taarifa ya mapokezi ya fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 69 kwa shule za sekondari na madarasa 127 ikiwa imetengwa jumla ya Tsh. 20,000,000/= kwa kila jengo/darasa. Kikao kilipitisha ujenzi huo ufanyike kwa kuzingatia muongozo uliotolewa wa single source ama mkandarasi na fedha hizo zitosheleze madarasa hayo kwani Halmashauri haina fedha zakuongezea kumaliza miradi hiyo na inatakiwa kumalizika kwa wakati na ubora uwepo



Scanned with CamScanner

pamoja na madawati pia. Jumla ya fedha zilizopokelewa ni 1,380,000,000 ikiwa ni ujenzi wa madarasa 69 kwa shule za sekondari na 2,540,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa madarsa 127 kwa shule za msingi. Aidha kiasi cha tsh 250,000,000 kimepokelewa kwa ajili ya ujenzi wa jingo la ICU na tsh 90,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba moja kwa watumishi watatu katika Hospitali ya Wilaya Tanganyika.

**AGENDA NA. HW/KTV/07/22/11/2021 – MENGINEYO**
Kikao kilijadili namna bora ya kulipa vikao vya bodi kwamba kila idara ama kitengo chenye mradi unaohitaji bodi kuketi basi watawajibika kuandaa malipo hayo na kuwalipa wajumbe.

**AGENDA NA. HW/MPN/07/03/11/2021 –KUFUNGA KIKAO**
Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 5:18 asubuhi.

**MUHTASARI HUU UMETHIBITISHWA NA KUSAINIWA NA**

**KATIBU**

**JINA** ....HARSON H. TENU....

**SAINI**....[signature]....

**TAREHE**....22/11/2021....

**MWENYEKITI**

**JINA**....H. Kitumba....

**SAINI**....[signature]....

**TAREHE** ....22.11.2021....



Scanned with CamScanner